

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu. Na. 025 – 2580272
Nukushi Na 025 – 2580044/71
Baruapepe: ded@mbozidc.go.tz



S.L.P. 3,
MBOZI.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.A.10/MDC/31 "C"/65

18/02/2021.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kupitia Kibali cha Ajira Mbadala kwa Watendaji wa Vijiji, Kibali chenye **Kumb.Na.FA.170/571/01/107** cha tarehe **21 Januari, 2021** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (UTUMISHI). Mkurugenzi Mtendaji anakaribisha maombi ya Watanzania wenye sifa na uwezo wa kuomba kazi ili kujaza nafasi za kazi ya **AFISA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III**.

1.0 AFISA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI 07

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anatakiwa awe na cheti cha kufaulu Kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI) na waliohitimu mafunzo ya Cheti (Astashahada) katika fani zifuatazo: Utawala, Uongozi na Usimamizi wa Fedha, Sheria, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

1.2 KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- ii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- iii. Kiongozi wa wataalam (watumishi wa serikali) katika kijiji.
- iv. Mhasibu (Afisa masuuli) na Mtendaji Mkuu wa kazi za kila siku za Serikali ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Taratibu zinazotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- vi. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- vii. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.

- viii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- ix. Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.

1.3 Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya Mshahara TGSB.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala ya vyeti vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- v. Picha moja "Passport Size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- vi. Testimonials, "Provisional Results" "Statement of Results" Hati za matokeo ya Kidato cha Nne na Sita, yaani FORM IV AND FORM VI. RESULTS SLIPS hazitakubaliwa.
- vii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 04/03/2021 saa 09:30 Alasiri. Aidha tangazo hili linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ambayo ni: www.mbozidc.go.tz, **Sekretariat ya Ajira na kwenye Mbao za Matangazo.**
- viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili fasaha au Kiingereza fasaha na yatumwe kupitia posta kwa anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI,
S.L.P 3,
MBOZI.**

Imetolewa na.



Hanji Y. Godigodi
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MBOZI.**